

KWENYE MSTARI, KAA TAYARI, ANZA!

Hapa kuna baadhi ya mambo unayoweza kufanya ili kukusaidia ujiandae kwa ajili ya Wasichana au Wavulana. Je, unaweza kupata mambo manne yanayofuatana?

 <p>Weka alama kwenye maandiko yako.</p>	<p>Zungumza na mtu ambaye yawezekana ana wasiwasi kuhusu kuhama kutoka darasa la Msingi.</p>	 <p>Ning'iniza juu nyumbani andiko unalolipenda.</p>	<p>Shiriki ushuhuda wako na mtu.</p>
<p>Mwombe askofu wako au rais wa tawi nakala yako ya <i>Kwa Ajili ya Nguvu kwa Vijana: Mwongozo wa Kufanya Chaguzi</i>.</p>	 <p>Pamba daftari la kwenda nalo darasani.</p>	<h2>Nafasi ya Wazi</h2>	 <p>Andika ujumbe wa shukrani kwa mwalimu wa Msingi</p>
<p>Soma maswali ya usaili wa kibali cha hekaluni.</p>  <p>(Unaweza kuyapata katika ukurasa wa 37 wa gazeti la <i>Rafiki</i> la mwezi Novemba 2022.)</p>	<p>Mwulize mtu kuhusu darasa la Wavulana au Wasichana likoje.</p>	<p>Mwombe mshiriki wa darasa lako aende na wewe kwenye darasa lako jipya.</p>	<p>Andika matarajio yako katika darasa la Wasichana au Wavulana.</p>
<p>Kutana na kiongozi kutoka kwa Wasichana au Wavulana.</p>	 <p>Andika mambo mawili unayotaka kujifunza katika darasa la Wasichana au Wavulana.</p>	<p>Soma makala katika gazeti la <i>Kwa Ajili ya Nguvu kwa Vijana</i>.</p>	 <p>Mwulize kiongozi wako mpya kuhusu shughuli za darasa. Ziandike kwenye kalenda yako!</p>

VIELELEZO NA COLLEEN MADDEN

KUHAMIA DARASA LA WAVULANA NA WASICHANA

Je, utakuwa na miaka 12 mwakani? Haya ndio baadhi ya mambo ya kuisimua.

Gazeti Jipya

Kwa Ajili ya Nguvu kwa Vijana ni gazeti kama lilivyo gazeti la *Rafiki* lakini hili ni kwa ajili ya Wavulana na Wasichana! Limejaa hadithi kuhusu vijana kote ulimwenguni ambao humfuata Yesu Kristo, kama vile wewe.

Mwongozo wa Kufanya Chaguzi

Kwa Ajili ya Nguvu kwa Vijana: Mwongozo wa Kufanya Chaguzi ni kijitabu kinachoweza kukusaidia uchague yaliyo mema. Kina maswali na majibu ili kukusaidia wewe umfuate Yesu Kristo na ujitayarisha kwenda hekaluni.



Shughuli Zaidi

Katika madarasa ya Wasichana na Wavulana, mnaweza kufanya shughuli za burudani pamoja na vijana wengine katika tawi au kata yako. Unaweza pia kuweka malengo kwa ajili ya programu za Watoto na Vijana ili kujifunza mambo mapya na kufanyia kazi vipaji vyako.